**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MREJESHO WA KILICHOZUNGUMZWA KWENYE UJUMBE WA MWAKILISHI MAALUM WA KATIBU MKUU WA JUMUIYA YA MADOLA, DKT. LAZARUS CHAKWERA, JUU YA MATUKIO YAMAUAJI, KUJERUHI NA UHARIBIFU WA MALI, OKTOBA 29, 2025 NCHINI TANZANIA**

**Dar es Salaam, April 17, 2026**

**Tarehe:** Ijumaa, 17 Aprili 2026
**Muda:** Saa 11:00
**Ukumbi:** TWAWEZA AFRIKA MASHARIKI

## Muhtasari

Lengo la tukio hili ni kufanya kikao cha kutoa mrejesho kwa maslahi ya umma, kwa vyombo vya habari, mashirika ya kiraia, wanataaluma, wanasheria, na watu wengine walioshiriki au wenye nia ya kujua maudhui ya mashauriano baina ya wadau na Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola katika mkutano wa mashaauriano uliofanyika Aprili 11, 2026 katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi za Umoja waMataifa, Jijini Dar es Salaam. Mjumbe huyo amekuwa nchini Tanzania tangu April 8 kwa ajili ya kutathmini na kukusanya data na taarifa za matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali kuhusiana na uchaguzi wa tarehe 29 Oktoba 2025. Kikao cha mrejesho kilifanyika katika ukumbi wa mikutano wa TWAWEZA AFRIKA MASHARIKI – Ni SiSi.

## Wazungumzaji Wakuu

1. Bi. Rosemary Mwakitwange – Mwenyekiti, CCCP/TG-MSG
2. Bubelwa Kaiza – Mratibu, Tanzania Transparency Forum
3. Deus Kibamba – Mtaalamu huru, wa Diplomasia na Utatuzi wa Migogoro
4. Dkt. Azaveli Lwaitama – Mtaalamu huru, wa Stadi za Mawasiliano na Tafakuri Tunduizi

Kila mzungumzaji anatarajiwa kuwapa wasikilizaji taarifa fupi kuhusu uchunguzi na hoja walizowasilisha wakati wa vikao vya Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, kuhusu uchunguzi wa matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025.

Mkutano huu wa waandishi wa habari unalenga kuujulisha umma wa Tanzania kuhusu uwepo na jukumu la ujumbe wa Jumuiya ya Madola nchini Tanzania, pamoja na kutoa ufafanuzi kuhusu

mijadala iliyofanyika wakati wa mikutano ya mashauriano kati ya Mjumbe Maalum na wadau, katika Ofisi za Umoja wa Mataifa jijini Dar es Salaam. Aidha, unalenga kujibu shauku halali ya umma ya kutaka kufahamu yaliyojiri katika vikao hivyo.

## Matokeo Yanayotarajiwa

Inatarajiwa kuwa kikao hiki cha mrejesho kitahamasisha Watanzania wenye taarifa muhimu kuhusu matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali wakati na baada ya uchaguzi wa tarehe 29 Oktoba kuwasilisha taarifa hizo kwa hiari kwenye utaratibu wa uchunguzi wa Jumuiya ya Madola. Hatua hii itasaidia katika maandalizi na uchapishaji wa ripoti yenye kuaminika, pamoja na kuchangia uwajibikaji unaozingatia Katiba na sheria, na kuendeleza mchakato wenye maana ya kuponya na kuwezesha maridhiano ya kitaifa.

## 1. Hotuba ya Ufunguzi – Mwenyelkiti

Bi. Rosemary Mwakitwange

Ni heshima yangu kuwatambulisha rasmi **Kundi la Wadau wa Utawala Bora Tanzania (TGMSG)** – muungano unaoongozwa na asasi za kiraia unaojumuisha wataalamu mashuhuri, wabobezi na viongozi wanaofanya kazi katika utafiti wa sera za umma, maendeleo ya asasi za kiraia, sekta binafsi, taaluma, vyombo vya habari na masuala ya utawala kwa ujumla, wakiwa na dhamira ya kuendeleza uadilifu wa kidemokrasia, uwajibikaji na maendeleo jumuishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 1.1 Muhtasari wa Kihistoria

Kundi la TG-MSG ni jukwaa la kisekta mbalimbali la utawala bora lenye paneli tano za kimaudhui zinazotoa mwelekeo wa kimkakati, usimamizi wa kitaalamu, na uwajibikaji kwa Timu ya Usimamizi wa Programu (PMT) inayosimamiwa kitaalamu.

Lilianzishwa mwezi Novemba 2025 na watafiti, wataalamu na viongozi wa asasi za kiraia Tanzania, ikiwa ni mwitikio wa wasiwasi uliotokana na ukiukwaji wa haki za binadamu na matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali wakati na baada ya uchaguzi wa tarehe 29 Oktoba 2025.

TG-MSG imejizatiti kuhamasisha na kuratibu wadau wa kitaifa, kikanda na kimataifa ili kushirikiana kurejesha amani endelevu, usalama na utawala wa kidemokrasia nchini Tanzania.

Muundo wa TG-MSG umebuniwa kuhakikisha mgawanyo wazi kati ya uongozi na usimamizi; uongozi wa kimkakati wa pamoja; utaalamu wa kina katika maeneo ya kimaudhui; uwajibikaji na uadilifu wa kifedha; pamoja na uendelevu wa taasisi zaidi ya afua moja. Sisi wajumbe wa ujumbe huu tunawakilisha Paneli ya Uwazi wa Dhana na Maudhui (CCCP) ya TG-MSG.

## 1.2 Muundo wa Uongozi

TG-MSG inaendeshwa kupitia muundo wa paneli tano za kimaudhui, ambazo ni: Paneli ya Uwazi wa Dhana na Maudhui (CCCP); Paneli ya Utafiti, Utetezi na Vyombo vya Habari (RAMP); Paneli ya Uhamasishaji na Mitandao (MONP); Paneli ya Uhamasishaji Rasilimali na Usimamizi wa Bajeti (BOP); na Paneli ya Ufuatiliaji, Tathmini, Uwajibikaji na Kujifunza (MEALP).

Tupo tayari kutoa taarifa zaidi kuhusu TG-MSG pale itakapohitajika. Tunapokutana leo, ingawa tuna uelewa wa jumla wa muktadha wa mkutano huu, tunaomba kwa unyenyekevu kufahamishwa kuhusu mbinu na njia zinazotumiwa na Jumuiya ya Madola katika kushirikiana na wadau nchini Tanzania kuhusiana na matukio ya tarehe 29 Oktoba. Hoja yetu kuu, na ambayo tungependa kuchangia, ni aina na ubora wa washiriki, uwigo wa kijiografia, pamoja na marudio ya mikutano ya wadau ili kuhakikisha timu yenu inapata mchango mpana na sahihi wakati wa uwepo wake hapa nchini.

## 1.3 Maeneo Yanayopendekezwa kwa Uchunguzi

Mheshimiwa Mjumbe Maalum, ingawa tunaelewa kuwa ziara yako nchini Tanzania imejengwa juu ya mamlaka ya Kundi la Mawaziri la Jumuiya ya Madola (CMAG), kama ilivyoainishwa katika taarifa yake ya tarehe 7 Machi 2026 – iliyokaribisha dhamira ya Tanzania kupokea na kuwezesha ziara na kazi ya Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu – na hivyo ratiba yako ya sasa huenda tayari imepangwa, TG-MSG, kwa kuzingatia maarifa na uzoefu wa ndani, inapenda kushirikisha timu yako ufahamu kuhusu chimbuko la matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali au uhasama unazohusiana na uchaguzi uliofikia kilele tarehe 29 Oktoba 2025. Tofauti na mienendo ya kawaida ya ushindani wa kisiasa katika uchaguzi, chama tawala cha dola, ambacho pia ni chama kilichopo madarakani, kilikiuka Katiba, sheria za uchaguzi na taasisi za usimamizi wa uchaguzi.

Aidha, tungependa kushirikisha timu ya uchunguzi ya Jumuiya ya Madola kuhusu maeneo kumi na moja (11) yaliyoathirika zaidi na matukio ya tarehe 29 Oktoba 2025. Matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali na ukatili vilijitokeza kwa kiwango kikubwa katika maeneo ya Geita, Katoro, Iringa, Tarime, Kahama, Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Tunduma na Bunda. Tunashauri kwa unyenyekevu lakini kwa msisitizo kuwa timu ya uchunguzi itembelee maeneo hayo na kukusanya ushahidi, hususan kufanya mikutano ya utafiti wa ukweli na viongozi wa dini wa maeneo husika, miongoni mwa wengine. Pia tunashauri afua zifikie maeneo yaliyo nje ya miji mikubwa ili kuhakikisha ushirikishwaji mpana.

## 1.4 Walengwa

Ili kuelewa muktadha wa matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali baada ya uchaguzi, kuna ushahidi unaoonyesha kuwa vijana, wanaotambulika kama kizazi cha Gen-Z, ndio walioathirika zaidi – wengi wao walijeruhiwa au kuuawa kwa kupigwa risasi, na miili yao haikuweza kupatikana kwa ajili ya mazishi yenye heshima. Aidha, vijana 2045 walikamatwa na kufunguliwa mashtaka ya uhaini, ingawa kufikia Desemba 2025, mashtaka 1151 yalifutwa kwa kukosa ushahidi (LHRC, 2025).

Mheshimiwa Mjumbe Maalum, Watanzania waishio ughaibuni (Diaspora) ni kundi jingine muhimu la kisiasa lililoathiriwa na matukio ya Oktoba 29. Hivyo, TG-MSG inaomba kwa unyenyekevu timu ya uchunguzi ya Jumuiya ya Madola iwafikie kundi hili, angalau kupitia moja ya makundi yao yanayosikika zaidi; Sauti ya Watanzania (SyW).

## 1.5 Mbinu dhidi ya Maudhui

Mheshimiwa Mjumbe Maalum,

Katika TG-MSG, kwa makusudi tumechagua kuelekeza ushiriki wetu katika mbinu na mchakato wa uchunguzi wa ujumbe wenu badala ya matokeo ya moja kwa moja ya uchunguzi huo. Hii inaakisi imani yetu kwamba mbinu thabiti, huru na yenye uwazi ya utafiti wa ukweli itapelekea hitimisho lenye kuaminika na mapendekezo yenye tija kwa hatua za marekebisho.

Tunatambua kwa heshima kwamba, endapo Serikali ya Tanzania itachukuliwa na wananchi wengi kuwa na wajibu kwa matukio ya tarehe 29 Oktoba 2025, taswira yoyote ya ukaribu au upendeleo kati ya ujumbe huu na Serikali inaweza kuhatarisha uaminifu, umuhimu na imani ya umma kwa ujumbe huo.

Kama wawakilishi wa wigo mpana wa asasi za kiraia, tunaeleza imani yetu kwako na timu yako. Ni matumaini yetu ya dhati kwamba ujumbe huu utafikia malengo yaliyokusudiwa—na hivyo kukidhi matarajio ya Watanzania na kusaidia kuweka msingi imara wa mchakato wa kweli wa uponyaji wa kitaifa.

## 1.6 Hitimisho

Ninapohitimisha waraka huu, niruhusuni kusisitiza tena yale ambayo TG-MSG inaona kuwa ni matarajio ya Watanzania kutoka katika uingiliaji wa Jumuiya ya Madola. Watanzania wanataka kujua:

1.6.1 Ni nani aliyetoa amri kwa watu wenye silaha "kupiga risasi na kuua raia" waandamanaji wasio na silaha waliokuwa wakitumia haki yao ya kikatiba kupinga kile walichoamini kuwa uchaguzi uliopangwa na kuchakachuliwa.

1.6.2 Uhalali wa amri ya Inspekta Jenerali wa Polisi kutangaza hali ya hatari tarehe 29 Oktoba 2025 – raia wasio na hatia waliotii amri hiyo waliwindwa na kuuawa wakiwa majumbani mwao kwa wakati mmoja nchi nzima; jambo ambalo haliwezi kuwa bahati mbaya.

1.6.3 Mamlaka au taasisi ya serikali iliyoratibu operesheni iliyolenga kudhibiti maandamano dhidi ya uchaguzi, tarehe 29 Oktoba 2025, kwa kuua raia.

1.6.4 Idadi na utambulisho (kwa kuzingatia jinsia, umri na maeneo wanakotoka) wa Watanzania waliouawa au kujeruhiwa wakati wa matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali wakati na baada ya uchaguzi wa tarehe 29 Oktoba 2025 na mara baada ya hapo.

1.6.5 Maeneo ambapo miili ya waliopotea kwa njia ya kutatanisha ilizikwa au kuchomwa moto, ili familia zao ziweze kufanya mazishi rasmi yenye heshima.

Tunashukuru ujumbe wa Jumuiya ya Madola kwa mchango wake katika juhudi za maridhiano nchini Tanzania.

## 2. Mrejesho wa Maudhui (Wazungumzaji Wakuu)

Bubelwa Kaiza

Mheshimiwa,

Mara tu baada ya Mwenyekiti kuwasilisha tamko letu la wazi, ningependa kutoa maelezo machache ya nyongeza na, pale inapofaa, mapendekezo. Haya yanatokana kwa sehemu na maswali ya Mheshimiwa Dkt. Lazarus Chakwera kuhusu hali na nafasi ya jamii ya kiraia nchini Tanzania, mfumo wa kisheria na kiudhibiti unaosimamia shughuli za kisiasa, pamoja na hali ya watu walioko kizuizini hadi sasa.

Kwa kutoa muktadha mfupi, nina uzoefu wa zaidi ya miaka 33 kama mtendaji na mchambuzi katika sekta ya asasi za kiraia. Mbali na mafunzo ya uzamili katika masuala ya NGOs, asasi za kiraia na harakati za kijamii, kazi yangu imehusisha kufanya tafiti za mitazamo kuhusu rushwa na viashiria vya utoaji rushwa; kusaidia kuanzishwa kwa mitandao ya usimamizi wa mapambano dhidi ya rushwa katika ngazi ya wilaya katika zaidi ya wilaya 78; kushiriki kuanzisha miungano ya kitaifa ya uangalizi wa uchaguzi unaofanywa na wananchi; na kushiriki kuanzisha na kuratibu Mtandao wa Amani na Usalama wa Ukanda wa Maziwa Makuu (PeSeNet). Kwa sasa ninahudumu kama mshauri wa sera wa vuguvugu la RAIA Ni SISI—ikiwakilisha wakulima wadogo, wavuvi wadogo, wafugaji wadogo na wachimbaji madini wadogo, ambao kwa pamoja wanaunda takribani asilimia 92 ya wananchi wa Tanzania—huku pia nikiwa mratibu wa Kundi la Wadau wa Utawala Bora Tanzania (TG-MSG) kupitia Jukwaa la Uwazi Tanzania (TRAFO), ambalo ni taasisi mwenyeji wa TG-MSG.

Ni kwa msingi wa uzoefu huu ninawasilisha kwa heshima maoni na mapendekezo yafuatayo:

**2.1** Mazingira ya uendeshaji kwa NGOs nchini Tanzania yamebanwa na mfumo wa sera na sheria wenye vikwazo. Mifano muhimu ni pamoja na Sheria ya NGOs (Marekebisho ya 2019), Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari (2016), Sheria ya Takwimu (2019 na 2025), Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Kanuni za Maudhui Mtandaoni, 2020), na Sheria ya Makosa ya Mitandao (2015). Kwa pamoja, sheria hizi zinaweka vikwazo vikubwa kwa ukuaji, uhuru na ufanisi wa mashirika ya kiraia.

Kwa mfano, Sheria ya NGOs (Marekebisho) ya mwaka 2019 ina vifungu vinavyoonekana kuwa vya kibaguzi dhidi ya taasisi fulani, ikiwemo mashirika ya kidini, na haitambui kikamilifu NGOs kama taasisi endelevu. Usajili wake umewekewa kikomo cha miaka kumi, na upyaishaji wake unategemea maamuzi ya Msajili, hali inayosababisha kutokuwepo kwa uhakika wa mwendelezo wa taasisi.

Aidha, Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 imekosolewa kwa kudhoofisha viwango vya maendeleo kama vile vilivyoainishwa katika Sheria Mfano ya Upatikanaji wa Taarifa ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Zaidi ya hayo, mazingira ya uendeshaji yameathiriwa na changamoto za kiusalama, ikiwemo taarifa za kupotezwa kwa watu kwa lazima. Kufikia Agosti 2025, zaidi ya raia 200 wa Tanzania waliripotiwa kupotea—wakidaiwa kutekwa, kuteswa au kuuawa (Tanganyika Law Society, 2025).

Kwa ujumla, muktadha wa sasa wa kisheria, kisiasa na kiusalama unabanwa nafasi ya kiraia, unapunguza ushiriki wenye maana, na kudhoofisha uhuru wa msingi. Hii inaonesha umuhimu wa haraka wa kuhimiza mazingira wezeshi zaidi yatakayoruhusu NGOs kufanya kazi kwa uhuru, uendelevu na ufanisi mkubwa.

**2.2** Kuna nyakati kadhaa, kati ya mwaka 2023 na 2025, Rais Samia Suluhu Hassan alisikika na kunukuliwa na nyombo vya habari akiwa kwenye mikutano yake ya mara kwa mara na vyombo vya ulinzi na usalama, ikifanyika Dar es Salaam, Arusha, Dodoma au Kilimanjaro, akiwaambia askari polisi na hata jeshi, kuwa serikali ilikuwa imetenga bajeti ya mahsusi kwa ajili ya askari nyakati za uchaguzi mkuu 2025. Kisera na kisheria, mipango hiyo ilikuwa na mapungufu makubwa, kwa sababu, kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi, majeshi yote hayapaswi kujihusisha na shughuli za siasa. Matokeo ya kauli na ahadi za Rais Samia kwa vikosi vya ulinzi na usalama, ni pamoja na askari polisi kutoa kuingilia uchaguzi mkuu 2025 wakitoa maelekezo ya kipolisi nchi nzima kati ya mwezi Januari hadi Desemba 2025. Vitendo vya kipolisi vilidhihirika kupendelea Chama Cha Mapinzuzi au wagombea waliopitishwa na chama hicho dhidi ya wagombea wa vyama vya upinzani. Wakati na baada ya kampeini za uchaguzi polisi waliingilia hata majukumu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Polisi na vyombo vya ulinzi na usalama walitoa amri ambazo ni kinyume na sheria ya uchaguzi, namba 1/2024, kwa mfano kuzuia wagombea kurudisha fomu za uteuzi kwenye ofisi za INEC.

**2.3** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) inabeba sehemu ya uwajibikaji kwa matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali ya tarehe 29 Oktoba na mwanzoni mwa Novemba 2025. Chombo hicho kilitenda kinyume cha sheria kwa kukiuka Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 2024, hususan kwa kuanzisha Kanuni za Kamati za Maadili kwa namna isiyoendana na Kifungu cha 162 cha sheria mama. Hatua hii inaonekana ilifanyika kwa madhumuni—au angalau kwa matokeo—ya kuiondoa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa 2025. Uamuzi huu uliibua hasira kubwa miongoni mwa wananchi, hasa vijana wengi waliokiunga mkono chama hicho.

Aidha, INEC iliweka masharti ya mapema ya uthibitishaji kwa vyama vya siasa, na pale CHADEMA iliposimamia utii wa sheria, iliondolewa kushiriki katika uchaguzi mkuu.

**2.4** Vilevile, INEC ilikataa kutoa ithibati kwa mashirika na miungano huru ya waangalizi wa uchaguzi, hivyo kuwazuia kupanga na kufanya uangalizi wa uchaguzi kwa kujitegemea. Huu si mwenendo mpya; ulianza tangu uchaguzi wa 2020 ambapo taasisi hiyo hiyo ilikataa kutoa ithibati kwa makundi kama Tanzania Civil Society Consortium on Election Observation

(TACCEO), ambayo hatimaye ililazimika kurejesha fedha za wafadhili na kusitisha shughuli zake.

Kwa kuzingatia ripoti za waangalizi wa uchaguzi, ikiwemo wa Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), zinazoashiria kuwa hakukuwa na uchaguzi wa maana siku ya kupiga kura, masuala haya yanahitaji kuangaliwa kwa uzito. Tunapendekeza ujumbe wa Jumuiya ya Madola ulibainishe wazi suala hili na kuzingatia mapendekezo madhubuti ya mageuzi.

**2.5** INEC pia inaonekana kuwezesha mfumo uliodhoofisha matakwa halisi ya wapiga kura, kama inavyoonekana katika kutokuwiana kati ya Sheria ya Uchaguzi—Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024—na Kanuni za Uchaguzi za mwaka 2025. Kifungu cha 102(d) na (e) kinataka kura zihesabiwe na matokeo kutangazwa katika kila kituo cha kupigia kura; mawakala wa vyama kupewa nakala za matokeo; na matokeo kubandikwa wazi.

Hata hivyo, Kanuni ya 52 inalenga zaidi kurekodi na kusafirisha fomu za matokeo kwenda vituo vya majumuisho bila kuhakikisha uwazi katika vituo vya kupigia kura. Tofauti hii inaleta wasiwasi mkubwa kuhusu uadilifu wa mchakato wa uchaguzi na inaashiria uwezekano wa udanganyifu wa makusudi. Tunapendekeza hatua za marekebisho na uwajibikaji zichukuliwe.

**2.6** Mahakama pia inaonekana, kwa mtazamo wa wadau wengi, kuchangia mapungufu ya mchakato wa uchaguzi wa 2025. Mwezi Mei 2025, raia wawili waliwasilisha maombi Mahakama Kuu wakitaka uingiliaji wa kisheria. Hata hivyo, mwezi Julai 2025, maombi hayo yalitupiliwa mbali kwa hoja kwamba wapiga kura hawana maslahi ya kisheria ya kutosha kushitaki katika masuala ya uchaguzi.

Vilevile, Shauri la Mapitio ya Kisheria Na. 32537 la mwaka 2025—lililopinga uamuzi wa Rais kuunda Tume ya Uchunguzi kuhusu matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali za uchaguzi—nalo lilitupiliwa mbali. Nakala za maamuzi hayo zimeambatishwa kwa marejeo.

Maoni haya yanatolewa kwa nia ya ushirikiano wa kujenga, yakilenga kusaidia mchakato wa uchunguzi ulio huru, wenye kuaminika na wenye matokeo chanya.

Deus Kibamba

Baada ya mapokezi na ukaribisho mzuri, timu ya TG-MSG iliruhusiwa kuingia katika chumba cha mkutano cha Mjumbe Maalum. Utambulisho ulifanyika kwa pande zote mbili, ukianzia na ujumbe wa Mjumbe Maalum wa Jumuiya ya Madola. Kwa upande wetu, timu ya TG-MSG ilitumia fursa hiyo kulitambulisha kundi na pia kuainisha wasifu wa wajumbe wanne waliokuwepo: Rosemary Mwakitwange, Bubelwa E. Kaiza, Deus Kibamba na Azaveli Feza Lwaitama.

Nilikuwa wa tatu kupata nafasi ya kuzungumza na kutoa maoni yangu. Nikiendeleza hoja zilizowasilishwa katika hotuba za ufunguzi na utangulizi zilizotolewa na Rosemary na Bubelwa,

mchango wangu ulijikita katika kujibu orodha ya maswali yaliyowasilishwa kwetu na Mjumbe Maalum. Iliwasilishwa kwamba nafasi ya kiraia nchini imebanwa sana. Kuhusu hatua za mbele, ilipendekezwa kwamba ujumbe utoe mapendekezo yafuatayo:

**2.7** Tanzania inapaswa kuzingatia kuanzishwa mara moja kwa mpangilio wa serikali ya mpito ya muda, ili kuruhusu mageuzi makubwa kupangwa na kutekelezwa kwa pamoja na wadau wote wa kisiasa. Mageuzi hayo hayawezi kufanikiwa iwapo yatasimamiwa upande mmoja chini ya uratibu wa hali iliyopo sasa (yaani muunganiko wa CCM–serikali–vyombo vya usalama). Mwelekeo wa ukiritimba wa chama tawala umejenga utamaduni wa majivuno uliopitiliza, jambo ambalo limekuwa kero kubwa kwa umma. Kwa hatua za mbele, wadau wote muhimu wa demokrasia wanapaswa kuwakilishwa ipasavyo katika utekelezaji wa mageuzi yoyote yatakayokuja.

**2.8** Uchunguzi wa kitaalamu wa kisayansi (forensic investigation) unahitajika kufanyika mara moja badala ya kusubiri, ili kubaini ukweli kuhusu majina, idadi na mahali walipo watu wote waliopotea kabla, wakati na baada ya tarehe 29 Oktoba. Ni kupitia mchakato huu pekee ndipo idadi halisi ya waathirika, waliokufa na utambulisho wao unaweza kuthibitishwa. Uchunguzi huu unaweza kutumia teknolojia za DNA na satelaiti. Maeneo yanayoshukiwa kuwa na makaburi ya pamoja yanaweza kuwa mwanzo wa utekelezaji wa uchunguzi huo.

**2.9** Kuna haja ya kuwaachia huru mara moja watu wote wanaodhaniwa kuwa wahusika ambao kwa sasa wanashikiliwa baada ya kuwekwa kizuizini, kutekwa au kupotezwa kwa lazima kabla, wakati na baada ya tarehe 29 Oktoba 2025. Hili ni sharti muhimu la awali katika kuhakikisha mchakato shirikishi wa urejeshaji wa hali ya kawaida, na litasaidia kulainisha maandalizi ya mazungumzo ya upatanishi, uponyaji wa kitaifa na mageuzi ya Katiba.

**2.10** Mchakato wa mageuzi ya Katiba unahitajika kwa dharura. Mchakato huu unapaswa kuwa unaomlenga mwananchi, shirikishi na jumuishi ili kuepuka kunaswa tena na tabaka la kisiasa. Kazi zilizofanywa hapo awali kama rasimu za Tume ya Mabadiliko ya Katiba na Bunge Maalum la Katiba zinaweza kuwa mchango mkubwa katika kuandaa rasimu ya mwisho ya Katiba (KATIBA) itakayothibitishwa kupitia kura ya maoni ya wananchi. Maoni mapya yanaweza kujumuishwa ili kusasisha rasimu hizo kutokana na muda mrefu uliopita tangu mchakato huo kusimama mwaka 2014. Aidha, uhamasishaji mkubwa wa uelewa wa Katiba unaoongozwa na asasi za kiraia na wananchi unapaswa kufanyika kabla ya mchakato huo.

**2.11** Mabadiliko ya kina ya mfumo wa kisiasa na uchaguzi yanahitajika sana. Kwa sasa, uchaguzi hauakisi matakwa ya wapiga kura wa Tanzania. Mageuzi ya uchaguzi yaliyotekelezwa kwa nia mbaya au kwa juu juu yamepotosha madhumuni halisi ya uwepo wa uchaguzi. Zaidi ya hayo, rushwa, takrima na hongo katika chaguzi za ndani ya vyama na uchaguzi wa kitaifa zimeharibu thamani ya mchakato huo. Kwa muhtasari wa kauli za SADC, AU na Taasisi ya Mbeki, Tanzania haikuwa na uchaguzi halisi mwaka 2025. Bila kufanya mabadiliko makubwa ya mfumo wa uchaguzi, nchi iko katika hatari ya kukumbwa na machafuko na mauaji kwa kiwango kikubwa zaidi, kinachoweza kufanana na mauaji ya kimbari katika siku zijazo.

**2.12** Kwa muhtasari, nilisisitiza umuhimu wa kushirikiana kwa karibu na taasisi zenye kuaminika pamoja na watu mashuhuri wanaoheshimika ili kuiwezesha timu ya Jumuiya ya Madola kufikia, kukutana na kusikiliza watu kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania—sio tu Dar es Salaam na Dodoma. Ushirikiano huu ni muhimu katika kukusanya ushahidi halisi na wa kuaminika kuhusu matukio ya tarehe 29 Oktoba 2025 na siku tatu hadi sita zilizofuata, hususan kuhusiana na mauaji na majeruhi ya vijana wasio na silaha yaliyosababishwa na vyombo vya dola.

Taasisi na watu muhimu ni pamoja na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Sheikh Issa Ponda, Askofu Benson Bagonza, Askofu Emmaus Mwamakula, na Askofu Joseph Gwajima.

Aidha, iwapo Timu ya Uchunguzi wa Ukweli ya Jumuiya ya Madola inalenga kuandaa ripoti itakayokubalika na kuaminiwa na Watanzania wengi, ni lazima iepuke taswira yoyote ya kuonekana kuwa inaegemea au imejikita ndani ya miundo ya serikali au chama tawala.

**2.13** Ili kuelewa chanzo cha matukio ya tarehe 29 Oktoba 2025 na siku zilizofuata, ni muhimu kuchunguza masuala ya kimuundo ya utawala—hususan athari zake kwa haki ya wananchi kujitawala. Hii inajumuisha kukosekana kwa viongozi wanaochaguliwa katika ngazi za kata, tarafa, wilaya na mikoa, sambamba na uteuzi mkubwa wa viongozi wa kiutendaji—kama vile Watendaji wa Vijiji/Mitaa, Watendaji wa Kata na Tarafa, pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri—unaofanywa na serikali kuu.

Mkusanyiko wa mamlaka ya uteuzi katika Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano unaonekana kufanana, au hata kuzidi, ule wa Gavana wa kikoloni, ambaye pia alikuwa akiteua viongozi wa ngazi za mikoa na wilaya, japokuwa kulikuwepo kwa kiwango fulani cha mamlaka ya wenyeji.

**2.14** Pia nilisisitiza kuwa kutatua mkwamo wa kisiasa uliopo nchini Tanzania kunaweza kuhitaji ushiriki wa mpatanishi wa nje mwenye kuaminika—kama vile Dkt. Naledi Pandor chini ya mwamvuli wa SADC—ili kuwezesha mchakato wa mazungumzo ya kujenga na yenye kuaminika.

**2.15** Mwisho, nilieleza umuhimu wa kujifunza kutoka nchi kama Malawi—na kwa kiasi fulani Kenya na Ghana—kuonesha kwamba chama tawala au cha ukombozi kinaweza kuachia madaraka ya dola kwa njia ya amani kupitia uchaguzi huru na wa haki na bado kikaendelea kuwa na uhalali wa kisiasa. Hili ni muhimu katika kupinga dhana iliyojengeka kwamba kupoteza madaraka kunamaanisha kutengwa kabisa kisiasa, mtazamo ambao mara nyingi hutumika kuhalalisha uchakachuaji wa uchaguzi.

**Mwisho**

## Imetolewa na:

1. Tanzania Transparency Forum (TRAFO), Taasisi Mwenyeji, Kiutawala, wa Tanzania Governance Multi-Stakeholders Group (TG-MSG)
2. Jukwaa la Katiba Tanzania
3. Concern for Development Initiatives in Africa (ForDIA), Taasisi Mwenyeji wa Kiutawala wa Vuguvugu la RAIA Ni SiSi, Tanzania
4. National Consortium of Civic Education in Tanzania (NACOCET)
5. Muungano wa Vyama Vya Wavuvi Tanzania (FUO)
6. Pastoralists Indigenous Non-Governmental Organisations (PINGOs) Forum

**Kwa ufafanuzi zaidi na taarifa kwa wahariri**

Taarifa hii imetolewa na makundi ya asasi za kiraia yaliyotajwa hapo juu na kuratibiwa na Tanzania Governance Multi-Stakeholders Group (TG-MSG), iliyoanzishwa mwezi Novemba 2025 na watafiti, wataalamu, na viongozi wa asasi za kiraia nchini Tanzania kwa lengo la kuratibu mwitikio dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu, mauaji, na matukio ya mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali kutokana na Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025.

TG-MSG imejizatiti kuhamasisha na kuratibu wadau wa kitaifa, kikanda na kimataifa ili kushirikiana katika kurejesha amani endelevu, usalama, haki na utawala wa kidemokrasia nchini Tanzania. Kwa taarifa zaidi, wasiliana na TG-MSG kupitia +255 639 365 465.